SEBHA UNIVERSITY JOURNAL OF HUMAN SCIENCES VOL.23 NO. 1 2024
DOI: 10.51984/JOHS.V23I1.3024

مجلة جامعة سبها للعلوم الإنسانية
Sebha University Journal of Human Sciences

Journal homepage: www.sebhau.edu.ly/journal/johs

# Lugha Na Utamaduni: Uhusiano Wa Kisemantiki Katika Methali Za Kiswahili Na Kiarabu

Laabidi Abdellatif[a]*

Idara ya Lugha ya Fasihi, Chuo Kikuu Huria Tanzania, Kinondoni, Dar es Salaam, Postikodi: 14111 15118, Tanzania

**Istilahi muhimu**
Kiarabu
Kiswahili
Lugha
Methali
Semantiki
Utamaduni

**IKISIRI**

Makala hii imejikita katika mtazamo mtambuka na linganishi wa taaluma za lugha na utamaduni. Lengo la makala hii ni kuonesha uhusiano kati ya utamaduni wa Mwarabu na Mswahili kupitia lugha ya Kiswahili na Kiarabu katika nyanja ya kiisimu. Inaainisha mfanano baina ya methali za Kiswahili na Kiarabu katika mawanda ya semantiki. Kwa kutumia nadharia ya Grice ya semantiki makusudio, makala hii inajenga hoja kuwa methali za Kiswahili na Kiarabu zinathibitisha uwepo wa uhusiano ambao unaashiria na kuthibitisha mwingiliano wa kitamaduni baina ya Waswahili na Waarabu. Imebainika kuwa methali za pande zote mbili zinashiriki mantiki kimuktadha kwa kuzingatia lengo la ujumbe wa methali husika. Data ya makala hii ilikusanywa kupitia mahojiano pamoja na upitiaji matini. Sehemu kubwa ya data iliyokusanya inajumuisha methali za Kiswahili na Kiarabu pamoja na maana zake. Pia wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili na Kiarabu wapatikanao jijini Dar es Salaam, Tanzania walihusika katika mahojiano. Walihojiwa juu ya maana na matumizi ya methali hasa katika nyanja ya familia na mfumo wa haki. Makala hii pamoja na umuhimu wake kitaaluma, inaweza kutumika katika kuimarisha uhusiano wa kiutamaduni na hata diplomasia baina ya Tanzania na mataifa ya Kiarabu.

# اللغة والثقافة: العلاقة الدلالية بين الأمثال العربية والسواحلية

عبد اللطيف لعبيد

شعبة اللغة والآداب، الجامعة الحرة بتنزانيا، كنوندوني، دار السلام، الرمز البريدي ١٤١١١١٥١١٨، تنزانيا

**الكلمات المفتاحية:**
الأمثال
الثقافة
الدلالة
العربية
السواحلية

**الملخص**

يقدم هذا المقال دراسة مقارنة في مجالي اللغة والثقافة بين اللغتين العربية والسواحلية بهدف إظهار العلاقة الوطيدة بين الثقافتين على المستوى اللغوي. فهذا المقال يبرز أوجه التشابه بين الأمثال السواحيلية والعربية من حيث الدلالة. وباستخدام نظرية جريس في جانبها الدلالي، يرى هذا المقال أن الأمثال السواحلية والعربية تؤكد وجود علاقة تفاعلية بين السواحلية والعربية. وقد تبين من خلال هذه الدراسة، أن الأمثال لدى الثقافتين تشترك في المنطق السياقي المبني على هدف إرسال رسالة مجتمعية ذات بعد ثقافي. فلقد تم جمع بيانات هذا المقال من خلال مقابلات وكذلك مراجعة بعض الوثائق والنصوص باللغتين العربية والسواحلية. وجدير بالذكر، أن معظم هذه البيانات السواحيلية والعربية ومعانيها تم العثور عليها من خلال قاموس الأمثال السواحيلية. كما شارك في المقابلات متحدثون باللغة السواحيلية والعربية في دار السلام، بدولة تنزانيا الاتحادية. ويمكن القول أن هذا المقال له أهمية اكاديمية وثقافية من اجل تعزيز العلاقات الثقافية وكذا الدبلوماسية بين تنزانيا والدول الناطقين باللغة العربية

## 1. Utangulizi

Lugha na utamaduni ni dhana mbili zinazofungamana kwa karibu kwa namna changamano. Kwa hakika, wataalamu wa isimu pamoja wataalamu wa athropolojia hupendekeza kuwa lugha na utamaduni haviwezi kutenganishwa (Tannen, 2006:333). Hakuna utamaduni bila lugha na hakuna lugha bila utamaduni. Ulimwenguni kote, lugha imeendelea kuwa kiungo muhimu zaidi katika utamaduni wowote. Ni

*Corresponding author:
E-mail addresses: laabidiabdellatif2023@gmail.com

Article History : Received 11 February 2024 - Received in revised form 29 May 2024 - Accepted 05 June 2024

chombo muhimu katika utamaduni wowote. Kwa mujibu wa Kassu (2018:105), utamaduni kama jumla ya mila, desturi na mitindo ya maisha ya watu wa jamii fulani ni kiungo muhimu katika kuutambulisha utamaduni fulani (Jiang, 2000). Hivyo kwa kuchunguza lugha ni sawa kabisa na kuchunguza utamaduni ambamo lugha husika hutumika. Makala hii inachunguza mwingiliano baina ya Kiswahili na Kiarabu katika nyanja ya semantiki kwa kutumia methali ambazo kiasili huwa na dhima kubwa kiutamaduni. Jumla ya methali nane (8) zimeteuliwa katika kuanisha uhusiano wa kiutamaduni kati ya jamii mbili kwa kuzingatia Kiarabu cha nchini Moroko na Kiswahili nchini Tanzania. Methali hizi nane zimegawanywa katika vipengele viwili vya utamaduni. Kila kipengele kina methali nne zinazoashiria mfanano na mwingiliano baina ya tamaduni na ustaarabu wa pande hizi mbili. Vipengele hivyo vinahusisha familia pamoja na masuala ya haki. Hivyo, kuna methali nne juu ya familia kama kipengele cha kitamaduni na kijamii. Pili, kipengele cha masuala ya haki kama wajibu wa kitamaduni na kimaadili kimechunguzwa kupitia methali nne za Kiswahili na Kiarabu. Makala hii inahitimisha kuwa mfanano na mwingiliano katika methali za Kiswahili na Kiarabu unaashiria uhusiano wa muda wa kihistoria katika tamaduni na lugha. Pia, kuna uhusiano wa karibu zaidi baina ya lugha na tamaduni zinazohusika na Waarabu na Waswahili na hivyo kwa kuchunguza uhusiano huu wa kiisimu makala hii imeweza kuthibitisha uhusiano wa kiutamaduni.

## 2. Malengo ya Utafiti na Nadharia Tete

Makala hii inatokana na utafiti uliokawa na malengo yafuatayo; Mosi, kubainisha methali za Kiswahili na Kiarabu katika nyanja za familia na mfumo wa haki. Pili kuchunguza mfanao wa kisemantiki katika methali hizo na tatu ni kung'amua kiwango cha mwingiliano wa kiutamaduni baina ya Waswahili na Waarabu kwa kutumia methali zilizobainishwa kupitia nyanja za familia na haki katika jamii. Kutokana na malengo haya, makala hii ilijenga nadharia tete zifuatazo; Mosi, Karibia methali zile zile hutumika kwa Waswahili na Waarabu katika kurejelea familia na mfumo wa haki? Pili, kuna mfanano wa kiwango gani wa kisemantiki katika methali za Kiswahili na Kiarabu katika nyanja za Familia na Haki? Tatu, methali hizi zinaashiria kiwango gani cha mwingiliano wa kiutamaduni baina ya Waswahili na Waarabu?

## 3. Mapitio ya kazi tangulizi

Tafiti nyingi tangulizi zimefanikiwa kuangazia uhusiano baina ya lugha ya Kiswahili na Kiarabu. Tafiti hizi zimefanikiwa kubainisha msingi wa ufanano na hata tofauti baina ya lugha hizi mbili katika nyanja mbalimbali za kiisimu. Nyanja tofauti za isimu zinahusisha leksikolojia (Gichuru, 2020), fonolojia na sarufi (Babusa 2019) na nyaja nyinginezo ikiwemo semantiki Shembilu (2005). Hata hivyo, Versteegh (2001) anaonesha kuwa tafiti nyingi hasa za kulinganisha juu ya makutano baina ya lugha na tamaduni za Kiarabu na lugha nyingine zimejikita hasa katika kujadili juu ya hali kutawala (utawala) kwa Kiarabu dhidi ya lugha na tamaduni nyingine. Mfano mmoja unaoelezea swala hili ni kupotea kwa lugha ya Kikoptiki katika Misri ya kale baada ya kumezwa na utawala wa lugha ya Kiarabu miongoni mwa wale waliokuwa wazungumzaji wa Kikoptiki. Kwa baadhi ya watafiti wameendelea kuwa na mtazamo huo huo katika uhusiano baina ya Kiswahili na Kiarabu. Hata hivyo, Shembilu (2005) anajadili juu ya michakato ya kisemantiki katika nomino za mkopo zenye asili ya Kiarabu na Kiingereza. Anabainisha kuwa nomino katika lugha kopaji huchakatwa katika viwango mbalimbali vya kiisimu ambapo moja ya michakato hiyo ni mchakato wa kisemantiki. Kwa kutumia nadharia ya sarufi amarifu, Shembilu anahitimisha kuwa mabadiliko ya kimaana ya nomino za mkopo yanatokana na namna jamii ya Waswahili wanavyotamia nomino hizo kutokana na mahitaji yao ya kimawasiliano. Anathibisha kwamba michakato hiyo inachangiwa kwa kiwango kikubwa na mahitaji ya kijamaa kwa namna ambayo utamaduni unahusika moja kwa moja.

Kuhusu methali, King'ei na Ndalu (1989) katika chapisho lao la Kamusi ya methali za Kiswahili wamefanikiwa kuainisha na kufafanua vyema methali nyingi za Kiswahili. Wametoa maana zaidi ya moja kwa kila methali. Pia, kila methali imeainishwa sambamba na methali yake linganishi, kwa mfano, "achanikaye kwenye mpini hafi njaa" mbali na maana pamoja na tafsiri yake kuwa ni "afanyaye kazi ya kulima kwa bidii hapatwi na shida ya njaa" kuna methali linganishi sambamba na maana ya methali hii ambayo ni "mgaagaa na upwa hali wali mkavu." Kamusi hii imefanikiwa kuainisha mantiki za methali za Kiswahili kwa kiwango kikubwa, hata hivyo Kamusi hii inakosa kipengele muhimu juu ya asili ya methali hizi pamoja na uhusiano wake na utamaduni wa Mswahili . Kwa msingi huo, makala hii inashughulikia uhusiano uliopo baina ya methali za Kiswahili na utamaduni wa Mswahili kwa pamoja na uhusiano wake na lugha na utamaduni wa Kiarabu ikiwa imethibitika kuwa Kiswahili na Kiarabu vina mwingiliano mkubwa kiisimu.

## 4. Nadharia ya Grice: Semantiki Makusudio (Grecian Intention-based Semantics)

Makala hii inaongozwa na nadharia ya Grice ambayo inaweza kuitwa 'semantiki makusudio' (Intention-based Semantics). Nadharia hii ilianzishwa na Profesa Paul Grice mwaka 1957 na kisha kuiboresha mwaka 1969 (Grice, 1957 & 1969). Katika nadharia hii, Grice anazungumzia maana za maneno au matamshi zinazotegemea kusudi. Kimsingi kusudi hilo linatambuliwa na utamaduni. Grice anaelezea maana isiyo ya asili kulingana na wazo la makusudi ya wazungumzaji (Black, 1973). Hata hivyo, Bräger (2020), anadai kuwa nadharia ya Grice (semantiki makusudio) ina vipengele viwili vya uchambuzi. Kipengele cha kwanza cha nadharia ya Grice ni Maana ya msemaji au maana ya matamshi. Katika hatua hii nadharia hii inahusu kile msemaji anakusudia kufikisha kwa msikilizaji, kwa nia yake ya mawasiliano, wakati wa kutamka sentensi fulani kwa wakati fulani. Kipengele cha pili kwa mujibu wa Chuo Kikuu cha Washington (2012), maana ya matamshi ya kulingana na hali ya kisaikolojia inayokusudiwa kuzalishwa katika hadhira. Semantiki hii hulenga katika matumizi ya lugha katika mawasiliano.

Kulingana na lengo la makala hii, vipengele vyote ni muhimu kwa kuzingatia kuwa methali huweza kuwa na maana ya wazi na iliyojificha au kufichwa. Kwa hiyo, katika kipengele cha pili cha uchambuzi, lengo ni juu ya taarifa za maelezo kuwa "Kwa kutamka x, S ilimaanisha kuwa P," kama katika mfano huu mtu akitamka "nataka kwenda kulala mapema.", anamaanisha kuwa "hataki kunywa kahawa." Kwa hivyo, katika mfano wa Kahawa, kwa kusema "Nataka kwenda kulala mapema" anamaanisha kuwa hataki kahawa, kwa sababu itamweka macho. Kwa hiyo, nia ni kujenga imani kwamba hataki kahawa angalau kwa sababu ya kutambua kwako kuwa kafeini ingemweka macho. Kwa kufupisha, usemi wa lugha hulingana na maana ya msemaji, daima una usemi wa pendekezo, kile kinachosimama kwa maana ya sentensi ya kisemantiki, na nia ya mtu anayetamka, ambayo ndiyo nia ya mawasiliano. Kwa kutumia nadharia hii, imewezesha kutambua au kung'amua ufanano wa kisemantiki baina ya methali za Kiswahili na Kiarabu kwa kuzingatia maana za methali kama ambavyo zinatumika katika lugha na tamaduni zote mbili.

## 5. Mbinu za Utafiti

Data ya utafiti huu imekusanywa kupitia mahojiano pamoja na mapitio ya matini. Katika mbinu ya mahojiano kulihitajika usampulishaji wa watoa taarifa. Sampuli ya utafiti huu ilipatikana kupitia usampulishaji kusudio. Usampulishaji kusudio ni mbinu ambayo watoa taarifa huteuliwa kwa kuzingatia sifa au kigezo maalumu kulingana na malengo ya utafiti. (Kelly 2010:317, Palinkas na wenzake 2015; Campbell na wenzake 2020). Katika mbinu hii, watoa taarifa wenye uwezekano mkubwa wa kutoa taarifa sahihi na muhimu huteuliwa. Ni mbinu ya usampulishaji yenye kutambua na kuchagua wahusika ambao wataleta ufanisi kwa kutumia rasilimali ndogo za utafiti. Mbinu hii ilitumika kutokana na kuwa data iliyohitajika katika utafiti huu ilitokana na watu wenye uelewa juu ya lugha ya Kiswahili na ya Kiarabu pamoja na tamaduni zake. Hivyo ni mtoa taarifa aliye na sifa ya kuelewa lugha hizi mbili na tamaduni zake ndiye alikuwa na nafasi kubwa ya kuhusika kwenye sampuli. Uelewa wa lugha na tamaduni hizi mbili ilikuwa moja ya kigezo kikuu cha uteuzi wa watafitiwa. Kwa. Hivyo, jumla ya watoa taarifa ishirini na tano walihojiwa. Kwa upande wa mbinu ya upitiaji wa matini nayo ilitumika. Matini muhimu zaidi yaliyotumika ni pamoja na Kamusi ya Methali za Kiswahili na (King'ei & Ndalu, 1989) pamoja na Kamusi ya Methali za Kiarabu (Sini & Soulaiman, 2010) na Kamusi ya methali za Kiarabu na Kiisilamu (Lunde & Wintle 1984). Matumizi ya matini haya yaliwezesha kufanya uthibitisho pamoja na ulinganishi wa data baina ya data kuhusu methali na mantiki zake zilizotokana na mahojiano pamoja na upitiaji wa matini.

## 6. Lugha na Utamaduni

Dhana za lugha na utamaduni hutegemeana. Lugha huzingatia maneno ya kutamkwa na maandishi huku utamaduni huzingatia utambulisho wa kundi fulani la watu (Tannen, 2006:333-34). Lugha na utamaduni hushiriki tabia na maadili ya kibinadamu au kundi maalum la watu. Kadiri dhana hizi mbili zinavyoendelea kukuwa, hushawishiana kwa njia ambayo ni vigumu kuzitenganisha. Utamaduni ni matokeo ya watu kutangamana ilihali lugha ni dhihirisho la kitamaduni la kundi fulani la watu. Kwa mujibu wa Gleason (1961), lugha sio tu matokeo ya utamaduni bali ni alama muhimu ya utamaduni. Kwa namna hii, lugha na utamaduni hutegemeana. Ukiondoa dhana moja, nyingine haiwezi kuishi. Lugha haiishii tu katika kuwasilisha mawazo na dhana. Inachukuliwa kuwa mfumo wa ishara unaounda na kuunda hali halisi. Mambo haya ni pamoja na utambulisho, mitazamo, na maadili, ambayo kwa hakika, ni sehemu ya utamaduni. Kwa mujibu wa Condon (1973), utamaduni unaweza kufafanuliwa kama njia ya maisha. Utamaduni una aina nyingi za mwelekeo ikijumuisha mawazo, desturi, ujuzi, sanaa na zana ambazo zina sifa ya kikundi cha watu katika kipindi fulani cha muda; pia ni imani, maadili, na vitu vya kimwili vinavyounda njia yetu ya maisha. Utamaduni huanzisha muktadha wa tabia ya utambuzi na ya kuathiri kwa kila mtu. Kwa upande mwingine, utamaduni unaweza pia kuchukuliwa kuwa tukio la mawasiliano. Kwa mfano, sanaa huwasilisha ujumbe wa msanii kwa hadhira yake. Ngoma pia huwasilisha ujumbe kwa hadhira. Sanaa na ngoma ni sehemu ya utamaduni wa kundi la watu na zina ujumbe ambao watu wanataka kufikisha kwa makundi mengine ya watu.

Pia, Kuo & Lai (2006), wanabainisha kuwa lugha ni taasisi ya kijamii, inayounda na kuundwa na jamii. Hivyo, uhusiano kati ya dhana hizi unaweza kuchambuliwa kupitia dhana iitwayo ‘’lugha ya uhusiano.’’ Maelezo rahisi ya dhana hii ni kwamba lugha huamua jinsi mtu anavyotazama ulimwengu. Au mtazamo wa mtu wa ulimwengu unalingana na lugha inayozungumzwa na mtu (Agha, 2007). Kwa hivyo, lugha ina athari ya moja kwa moja kwa utamaduni wa mtu. Ikiwa unataka kuelewa utamaduni fulani vizuri zaidi, unapaswa kujifunza kuzungumza lugha ya jamii au kikundi cha watu husika. Mara tu unapozungumza lugha hiyo, utakuwa na mtazamo tofauti kuhusu utamaduni wa mtu. Mawasiliano ni muhimu kujua jinsi mtu anavyotafsiri au kuutazama ulimwengu.

## 7. Semantiki

Semantiki ni kipengele muhimu cha lugha. Ni dhahiri ya kazi kuu ya lugha. Kimsingi, lugha ipo ili kufikisha "maana" au “ujumbe” wa kisemantiki. Hivyo semantiki inaweza kuwa kama msingi wa lugha maana inawakilisha utimilifu wa lengo kuu la mawasiliano kwa wazungumzaji wa lugha fulani (Haaheim, 2018). Kwa mujibu wa Leech (1985), semantiki ikiwa kama stadi ya maana ni muhimu katika taaluma za mawasiliano; na kadri mawasiliano yanavyozidi kuwa jambo muhimu katika kijamii, hitaji la kuelewa mawasiliano linakuwa kubwa zaidi na zaidi. Aidha, Crystal (1987), anasema kuwa semantiki ni utanzu wa isimu unaojikita kuchunguza maana katika lugha. Kwa maana nyingine, isimu ni stadi ya maana na utanzu wa isimu ambao huchunguza lugha za binadamu kwa viwango vya sauti, maneno, virai na hata sentensi.

Kwa upande wa Richards na wenzake (1985), semantiki ni stadi ya maana. Kwa upande mwingine, semantiki huchunguza maana iliyo wazi na ile iliyofichika (Tumaini, 2017). Katika ufafanuzi huu wa dhana ya semantiki ambao unahusisha uchanganuzi wa maana iliyo wazi na iliyojificha kunatoa na kufaa zaidi katika muktadha na malengo ya makala hii. Ufafanuzi huu unafaa zaidi kwa kuwa makala imejikita katika methali ambazo mara zote huwa na maana au ujumbe ulijificha. Katika makala hii, semantiki itatumika katika mtazamo wa maana za maneno, virai au sentensi huku ikihusishwa zaidi na methali pamoja na utamaduni ambapo nafasi yake katika tamaduni za Mswahili na Mwarabu itachunguzwa ili kung’amua mfanao baina ya lugha na tamaduni za Kiswahili na Kiarabu. Aidha, kwa mujibu wa Leech (1985), kuna aina saba za maana. Aina hizi zinahusisha maana ya kidhana, maana ya kiufafanuzi, maana ya kijamii na kuathiri, maana ya kutafakari na kuchanganya na maana shirikishi. Pamoja na nukuu hizi, dhana ya semantiki itatumika katika makala hii kama utanzu wa isimu unaojikita kuchunguza maana katika lugha. Na kwa sababu methali zina kawaida ya kuwa na maana au ujumbe uliyo wazi na iliyojificha basi semantiki katika makala hii itashughulika na maana zote zilizo wazi na zilizojificha.

## 8. Dhana, Sifa na Umuhimu Methali Katika Kiswahili na Kiarabu

Methali ni semi ambazo zina sifa mahususi za kujipambanua na semi zingine kutokana na sanaa yake, dhima yake kama kitambulisho, utamaduni na falsafa ya jamii inayohusika na usemi wenye ulinganifu na maisha ya wanadamu (Mtesigwa, 2013:9-10). Kwa upande mwingine, Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2004: 240), inafafanua dhana ya methali kama usemi wa kisanii wa kimapokeo unaofikiriwa na jamii kuwa kweli na unaotumiwa kufumbia au kupigia mfano au huwa umebeba maana pana kuliko maneno yenyewe yanayotumiwa. Ufafanuzi huu unafanana kwa kiasi fulani na ule wa Ngole na Honero (2004: viii), methali ni aina moja ya usemi mzito na ambao unakusudiwa kusema jambo maalumu lakini kwa namna ya fumbo. Usemi huu mzito mara nyingi hukusudiwa kumuonya, kumuongoza na kumuadilisha mwanadamu. Hata hivyo bado methali ni muhimu sana kwa jamii nyingi za Kiafrika katika kutimiza mahitaji kadha wa kadha ya kiutamaduni. Kwa mujibu wa King’ei (1989) kwa maana methali ni chombo maalumu cha mawasiliano katika jamii yoyote. Kwa ujumla methali zitazingatiwa katika makala hii kutoka katika mtazamo wa kiisimu zaidi kuliko fasihi pamoja na kwamba methali ni

moja ya utanzu muhimu wa fasihi.

Methali ni maneno rahisi ya jadi ambayo yanayowasilisha uhalisia au ukweli kwa jumla. Methali hufundisha maarifa na hekima na wakati mwingine hutoa ushauri au onyo dhidi ya jambo fulani kulingana na akili ya kawaida au uzoefu wa maisha ili kuchochea mawazo na fikra na pia kushawishi watu kujibu. Mara nyingi ni maneno ya mfano yanayotumiwa katika lugha maarufu katika kutafakari vipengele mbalimbali vya utamaduni na maisha, kama vile uchumi, siasa, jamii, haki na kadhalika. Methali zote hubeba hisia za kitamaduni au za kibinafsi au hisia za pamoja kuelekea mtazamo fulani au nafasi iliyotumiwa au kuundwa kwa mtindo rahisi wa lugha unaoelekezwa kwa watu fulani ili kuwapa mafunzo na mifano kutokana na uzoefu uliopita. Methali yoyote ina sifa na hubeba utamaduni fulani katika nafasi na wakati fulani kwa suala la maarifa, jamii na mazingira kwa sababu kila eneo hutambulika kulingana na asili yake ya kitamaduni na lugha, pamoja na tamaduni zake. Kwa sababu ya mwingiliano, ujumuishaji na ujamaa, methali zinazoashilia maingiliano zimeibuka kati ya tamaduni na tamaduni, zikiashilia mtagusano kati ya ustaarabu na ustaarabu na baina ya jamii na jamii haswa kupitia biashara na mabadilishano ya kitamaduni. Kimsingi, umuhimu wa methali huonekana katika ukweli kwamba:

- Methali ni muhimu kwa tamaduni zote

Kila tamaduni ina semi za methali ili kuunga mkono mila na maadili yake. Mara nyingi, methali na misemo huwasilisha maadili ya kitamaduni yanayokubalika katika jamii. Hapa kuna baadhi ya sababu kwa nini methali ni muhimu sana katika tamaduni: Methali kwa ujumla hutumiwa kutoa ushauri kwa wasikilizaji. Methali kama vile *Elimu haina mwisho* inaonekana kama ushauri wa kuwa kujifunza ni jambo lisilokuwa na ukomo.

- Methali hufundisha maadili na maadili jamii

Methali hufundisha umuhimu wa maadili mema. Pia methali hutoa maarifa na kueneza ufahamu juu ya maswala na mada fulani. *Umoja ni nguvu, utengano na udhaifu.* Methali hii ya Kiswahili ni kielelezo cha jinsi methali zinavyotumiwa kuwatia moyo watu na kuwatia nguvu ili kuungana na kufanya kazi kwa bidii.

- Methali hutumika kama maonyo kwa wasikilizaji

*Mafanikio sio mwisho, kushindwa si mbaya.* Methali hii inaonya mtu kutozingatia makosa bali juu ya kile kilichosababisha makosa; vinginevyo, mtu anaweza kurudia kosa lilelile (Dunmade, 2022).

Methali huwa na sifa fulani za kufanana, sifa hizo ni:

- Maneno rahisi na mafupi au vishazi au kauli;
- Rahisi kueleweka na kukaririwa;
- Mifano halisi na masomo;
- Ulinganifu Dhahiri na kwa usahihi;
- Alama na ishara zinazoashiria utamaduni maarufu katika jamii fulani.

Kwa kuzingatia sifa hizi, methali za Kiswahili na Kiarabu zinashiriki karibia sifa zote za aina moja kama inavyoainishwa katika nyanja mbili muhimu katika utamaduni wa Waarabu na Waswahili.

## 9. Familia

Familia kwa ujumla hutambuliwa kama kipengele cha mtandao mpana wa jamaa ambao unaunganisha mababu na uzao wa mtu. Ni muunganiko wa watu wawili au zaidi wanaohusiana kwa damu, ndoa, au kupitishwa, na kuishi katika makazi sawa (Fields and Casper 2001; Nam, 2004; 2). Lugha na tamaduni za Kiswahili na Kiarabu zinashiriki methali sawa katika nyanja ya familia. Zinazingatia familia kwa sababu ni kiini cha jamii yoyote kwa ujumla na kila mtu anaweza kuathirika ama kwa namna chanya au hasi kwa maana kwamba baba anaweza kumshawishi mtoto wake kwa urahisi na mama ana athari ya moja kwa moja kwa binti yake na pia watoto wanaweza kujifunza mambo mazuri na mabaya kutokana na ujamaa wao na wazazi wao.

- Baba na mtoto wa kiume, mama na mtoto wa kike;
- Mama mmoja mwema hushinda waalimu wa ulimwengu;
- Ndugu mbaya si sawa na jirani mwema/ Ndugu mbaya hushinda rafiki mzuri
- Ukitaka kusaidiwa nawe saidia wenzako. (Rejea jedwali 1)

**Jedwali 1:** Methali za Kiswahili na Kiarabu katika kipengele cha Familia

| **Methali ya Kiswahili** | **Methali Kifanani Katika Kiarabu na Tafsiri Zake** |
|---|---|
| 1. ***Baba*** na mtoto wa kiume, mama na mtoto wa kike | 1-الابن يشبه ابيه والبنت تشبه امها<br>a)- Alibn liabihi wa albinto liomoha<br>b)-Mtoto wa kiume anafanana na baba yake na binti anafanana na mama yake. |
| 2. ***Mama*** mmoja mwema hushinda waalimu wa ulimwengu | 2-الام مدرسة اد اعددتها اعددت شعب طيب الاعراف<br>a)- Al-Omo madrassa taybato alaarafo<br>b)- Mama ni shule, ukimtayarisha vyema, unatayarisha jamii yenye tabia njema. |
| 3. ***Ndugu*** mbaya si sawa na jirani mwema/ Ndugu mbaya ni bora kuliko rafiki mzuri | 3-خوك خوك لا يغرك صاحبك<br>a)- Khok khok laigharak sahabak<br>b)-Ndugu yako ni ndugu yako, rafiki yako hawezi kuchukua mahali pake. |
| 4. Ukitaka kusaidiwa nawe saidia ***wenzako*** | 4-الصدقة أولى بالاقارب<br>a)- Sadaqa awala balaqarib<br>b)- Kutoa sadaka kwanza kwa familia. |

*Chanzo: Abdelaatif (2024)*

Katika methali ya kwanza ya Kiswahili *Baba na mtoto wa kiume, mama na mtoto wa kike* na methali sambamba ya Kiarabu *Mtoto kiume anafanana na baba yake na binti anafanana na mama yake* zinawahimiza wazazi kuwa na maadili halisi ili watoto wao wafaidike na wazazi wao kwa kuzingatia maadili, tabia na mila. Mbali na hilo, tamaduni zote mbili katika methali zao zinamtazama mwanamke kama chanzo cha maarifa yaliyojaa maadili na fadhila. Katika methali ya Kiarabu, mwanamke anachukuliwa kama shule (Mama ni shule, ukimtayarisha, unatayarisha jamii yenye tabia njema) lakini katika Kiswahili mwanamke ni ulimwengu wa maarifa na utaalamu (***Mama*** mmoja mwema hushinda waalimu wa ulimwengu). Kwa ujumla, methali hizi zote zinaonyesha kuwa katika tamaduni zote mbili methali zinaangazia familia kama kitu muhimu katika kujenga vitalu vya jamii yoyote kwani familia hutumika kama kitalu kwa wananchi na inawajibika kwa maendeleo ya watoto ambao huathiriwa na

mazingira yao kwa mema au mabaya. Methali hizi katika kipengele hiki zinamchukulia baba na mama kama msingi halisi wa jamii na maadili yao yanaakisiwa katika jamii kwa ujumla.

Kwa upande wa udugu na mahusiano, methali za Kiswahili na Kiarabu (***Ndugu*** mbaya si sawa na jirani mwema/ Ndugu mbaya hushinda rafiki mzuri *dhidi ya* Ndugu yako ni ndugu yako, rafiki yako hawezi kuchukua mahali pake) zinasisitiza juu ya kudumisha uhusiano wa damu, yaani kati ya ndugu na jamaa badala ya kuzingatia majirani. Hata hivyo, kuna tofauti kati ya tamaduni hizi mbili kulingana na methali ya nne kwa maana ya upendo kwa maana kwamba Waarabu hutoa kipaumbele kwa jamaa katika kiwango cha msaada na kusaidia kimwili au kimaadili na hii inakwenda sambamba na mafundisho yao ya kidini. (Sadaka huanzia katika familia). Kinyume chake, Waswahili wakienda mbali zaidi na kusisitiza kuwa jamaa na marafiki pia wanapaswa kuwa sehemu ya hisani na msaada. Hii ni kutokana na kuwa Waswahili huitazama jamii kama chombo cha kilicho na usawa (Ukitaka kusaidiwa nawe saidia ***wenzako)***. Kwa ujumla, methali hizi zote za Kiswahili na Kiarabu zilizoelezwa katika kipengele hiki cha utamaduni katika kuashiria jukumu la wazazi, majirani na ndugu katika kuunda mahusiano ya kifamilia huchukulia familia kama msingi wa jamii kwa sababu ni mahali ambapo watu wa jamii husika wanaathirika zaidi binafsi. Methali hizi zinajadili umuhimu wa familia kama kitengo ambacho kina jukumu muhimu katika kutufanya watu bora kibinafsi na pia raia bora wa jamii zetu. Kama sehemu ya kiini cha familia, watoto, kulingana na methali hizi, hujifunza jinsi ya kuhusiana ipasavyo na wazazi wao na ndugu zao. Katika tamaduni hizi mbili, mahusiano ya kifamilia ni masomo ya maisha ambayo watoto hutumia katika kuunda uhusiano wao na ndugu na majirani. Familia ni muhimu kwa jamii kwa sababu ni msingi wa mahusiano ya kijamii.

## 10. Dhana ya familia katika Kiswahili na Kiarabu

Ni kweli kwamba tamaduni za Kiarabu na Kiswahili zinashiriki wazo kwamba familia ni msingi wa kila jamii kwa sababu taasisi hii ya kijamii hutoa watu tangu kuzaliwa hadi utu uzima, wakiwa na hisia ya umoja, kuhusiana, msaada wa kiuchumi, malezi, elimu, na ujamaa. Dhana ya familia inaweza kutafsiriwa tofauti na mtazamo wa mtu binafsi wa safu ya asili ya kitamaduni, na tamaduni hutofautiana katika maadili yake, tabia, na mawazo. Utamaduni wa familia ni mchanganyiko wa tabia, mila, madhumuni, maadili, imani, na uchaguzi wa familia husika. Mara nyingi huathiriwa na uzoefu, haiba, na ushawishi wa nje. Kimsingi, utamaduni unawakilisha jinsi watu wanavyojiona kama sehemu ya umoja wa kipekee wa kijamii na mwingiliano wa mawasiliano. Hatimaye, utamaduni hutumika kama moja ya nyanja kuu kwa watu binafsi kutafsiri na kutunga maagizo hayo, kama vile urithi, desturi za ndoa (kama vile mke mmoja na talaka) na imani juu ya jinsia. Kwa sababu hizi, kila familia ni zao la muktadha mkubwa wa kitamaduni na uchambuzi wa mawasiliano ya familia lazima ujumuishe utamaduni ili kutathmini mikakati madhubuti ya mawasiliano ili kutatua migogoro ya familia (Johnson & Zuckerman, 2013; 631–633).

Kuhusu mwingiliano wa kitamaduni kati ya jamii za Waswahili na Waarabu, ni kweli kwamba Waarabu walifika eneo la pwani kwa sababu za kibiashara. Mwingiliano huu ulisababisha ndoa na mahusiano mchanganyiko. Matokeo yake, jamii hizi mbili zinashiriki baadhi ya imani na mila za kitamaduni. Katika suala hili, tunaweza kuona seti ya maneno ya Kiarabu yakitumiwa kwa Kiswahili kufafanua ushirikiano huu wa kitamaduni, kama vile Binti, Baba, Mama, Bibi na Binamu. Istilahi za Kiarabu zinaonekana pia katika maneno yanayounda familia kama Kabila (qabila), Jamii (mujtamaa), Binafsi (nafs) na Jamaa (aqarib). (Rejea jedwali 2)

**Jedwali 2:**

| Kiswahili | | Kiarabu | | Kiingereza |
|---|---|---|---|---|
| ✓ | Binti | بنت | *Bint* | *Daughter* |
| ✓ | Baba | اب | *Ab* | *Father* |
| ✓ | Mama | ام | *Om* | *Mother* |
| ✓ | Bibi | جدة | *Jada* | *Grand mother* |
| ✓ | Binamu | ابن العام | *Ibnoam* | *Cousin* |
| ✓ | Kabila | قبيلة | *Qabila* | *Tribe* |
| ✓ | Binafsi | نفس | *Nafs* | *Personal* |
| ✓ | Jamii | مجتمع | *Mujtamaa* | *Society* |
| ✓ | Rafiki | رفيق | *Rafiq* | *Friend* |
| ✓ | Damu | دم | *Dam* | *Blood* |
| ✓ | Jadi | سلف | *Salaf* | *desturi* |
| ✓ | Binadamu | ابن العام | *Ibn am* | *human* |

*Chanzo: Abdelaatif (2024)*

## 11. Haki

Haki katika jamii kwa ujumla inapaswa hueleweka kama usawa kamili wa kiwango cha jumla cha faida na majukumu ya kila mwanajamii katika jamii husika (Ake, 2017). Baina ya wasahili na Waarabu, haki ni kipengele muhimu katika jamii na tamaduni hizi. Kwa sababu ya umuhimu wa mfumo wa haki, methali nyingi za Kiswahili na Kiarabu kuakisi haki. Kwa mfano, katika methali zifuatazo;

- Njia ya kupimia haki ni adhabu;
- Haki ya mtu haipotei, haigawanyiki/ Hukumu haijui nyumba maskini;
- Haki hushinda batili;
- Huja kwa msimu mvua/Jibu haina kifo. (Rejea jedwali 3)

**Jedwali 3:** Methali za Kiswahili na Kiarabu katika kipengele cha Haki

| Methali ya Kiswahili | | Methali Kifanani Katika Kiarabu na Tafsiri Zake |
|---|---|---|
| 1. | Njia ya kupimia haki ni adhabu; | 1-العدل اساس الملك<br>a)- Al-Adlo asaso almolk<br>b)-Haki ni msingi wa uongozi. |
| 2. | Haki ya mtu haipotei, haigawanyiki/ Hukumu haijui nyumba maskini; | 2-ماضاع حق ورائه طالب<br>a)- Madaa haqon waraoho talib<br>b)- Haki inayodaiwa, haiopotei. |
| 3. | Haki hushinda batili/ Siku zote haki na batili hujitenga kama mafuta na maji; | 3-الحق يعلى ولا يعلى عليه<br>a)- Al-haqo yuala wala yoala alihi<br>b)-Hakuna kilicho juu kuliko haki |
| 4. | Huja kwa msimu mvua/Jibu haina kifo. | 4-الحق ابان ابان<br>a) Al-Haq iban iban<br>b)- Haki hujitokeza mapema au baadaye. |

*Chanzo: Abdelaatif (2024)*

Kwa upande wa haki, tamaduni zote mbili zinatoa kipaumbele kwa haki kwa kuwa ndiyo chanzo cha amani na utulivu. Kwa Waarabu kulingana na methali ya kwanza (1), haki ni nguzo na pia msingi wa utawala. Vivyo hivyo, methali ya kwanza ya Kiswahili inaonyesha kuwa asili ya adhabu inahakikisha asili ya haki (Njia ya kupimia haki ni adhabu). Hivyo, kwa Waswahili adhabu ni kipimo kinachoweza kuamua nguvu au udhaifu wa sheria na haki. Hii inamaanisha kuwa

uundaji wa katiba na sheria unapaswa kuwa na sifa ya usahihi na usahihi ili kufanya adhabu na makosa viendane; Kila kosa linapaswa kuwa na adhabu ya kutosha ili kuwa jamii yenye haki. Methali ya pili ya Kiswahili na Kiarabu ni sawa na *Haki ya mtu haipotei, haigawanyiki/ Haki inayodaiwa, haipotei.* Pande zote zinasisitiza raia kutafuta njia za kutafuta haki zao kamili na methali ya tatu katika tamaduni zote mbili inaelezea kwamba haki iko juu ya kila kitu na siku zote haki hushinda madai yoyote mabaya au ya uongo kama ilivyoelezwa katika methali ya tatu (3) (Haki hushinda batili) kwa kuwa sauti ya haki hushinda sauti ya ufisadi kama ilivyoelezewa katika methali ya Kiarabu ya tatu (3) (Hakuna kilicho juu kuliko haki) wakati methali ya nne (4) ya Kiswahili (Huja kwa msimu mvua/Jibu haina kifo) inathibitisha kwamba, kwa sababu ya ushahidi wake, haki kamwe haiwezi kufa na huelea kama mafuta juu ya maji au inaonekana kama jua katika anga kama ilivyoelezwa katika methali nne (4) kwa Kiarabu (Haki hujitokeza mapema au baadaye).

## 12. Dhana ya Haki Katika Kiswahili na Kiarabu

Ni kweli kwamba dhana ya haki katika tamaduni zote mbili ina maana na uelewa sawa. Tamaduni zote mbili huona Haki kama kuwatendea watu kwa usawa na bila upendeleo, bila kujali asili yao, hadhi ya kijamii, au imani binafsi. Ni mfano wa haki na uadilifu, kukuza fursa sawa na kuhakikisha kwamba kila mtu anapata haki zake za msingi za kibinadamu. Dhana hii yenye sura nyingi kwa tamaduni zote mbili inajumuisha vipimo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na haki ya kijamii, haki ya kisheria, na haki ya usambazaji, kila moja ikishughulikia nyanja tofauti za usawa na haki. Tamaduni za Kiarabu na Kiswahili, kwa pamoja zinatambua umuhimu wa kutoa fursa sawa kwa watu wa jamii zote, jinsia, dini, na asili za kijamii.

Kipengele kingine cha msingi cha haki ni haki ya kisheria, ambayo inahusu matumizi ya sheria katika misingi ya haki. Jamii zote mbili zinasisitiza jamii ya haki ambayo watu wote, bila kujali misimamo yao au ushawishi, wako chini ya sheria na kanuni sawa. Pande zote zinatetea wazo kwamba haki ni kipofu, na hakuna mtu aliye juu ya sheria na kuheshimu dhana ya haki ambayo inahusu usambazaji wa haki wa rasilimali, utajiri, na fursa baina ya watu katika jamii. Kimsingi, tamaduni za Waswahili na Waarabu zinashiriki kanuni zile zile za haki, hasa Morocco na Tanzania. Hii ni kutokana na uhusiano wa kihistoria kati ya staarabu hizo mbili. Katika ulimwengu wa Kiarabu kwa ujumla na nchini Morocco hasa, haki na sharia zake nyingi hutokana na msingi wa kidini. Kwa hiyo, tamaduni hizi mbili zinashiriki misingi mingi ya kisheria kwa kuwa kuna jamii ya Waislamu nchini Tanzania pamoja na mawasiliano na ujumuishaji. Kwazo, haki inachangia mshikamano wa kijamii na maelewano ndani ya jamii. Ukosefu wa haki na ukosefu wa usawa mara nyingi husababisha migogoro na machafuko ya kijamii. Kwa hivyo, kulingana na methali hizi, haki inasimama kama dhana yenye nguvu ambayo inajumuisha usawa. Ina jukumu muhimu katika uongozi bora kwa kukuza uaminifu, kuhamasisha ujasiri, na kujenga jamii yenye usawa. Kama ilivyooneshwa katika jedwali la 4, maneno ya kisheria yaliyoshirikiwa kutoka Kiarabu na kuunganishwa kwa Kiswahili ili kuhakikisha mabadilishano ya kitamaduni kati ya tamaduni hizi mbili (Rejea jedwali 4).

**Jedwali 4**

| Kiswahili | Kiarabu | | Kiingereza |
|---|---|---|---|
| ✓ Hakimu | حكيم | hakimo | *Judge* |
| ✓ Mhalifu | مخالف | mkhalifo | *Criminal* |
| ✓ Hukumu | حكم | hokm | *Judgement* |
| ✓ Shahidi | شاهد | shahada | *Witness* |
| ✓ Sheria | شريعة | shariaa | *Law* |
| ✓ Haki | الحق | Haq | *Justice* |
| ✓ Madai | مدعي | modai | *Impeachment* |
| ✓ Kauli | قول | qawal | *Statment* |
| ✓ Mshtaki | مشتكي | Mshtaki | *Plaintiff* |
| ✓ Mshtakiwa | مشتكي به | Mshtaki bih | *Defendent* |
| ✓ Hatia | خاطئة | Khatia | *Guilty* |
| ✓ Dai | دعوة | dawa | *Claim* |
| ✓ Mkataba | مكاتبة | mokataba | *Contarct* |
| ✓ Mahakama | محكمة | mahakama | *Court* |
| ✓ Jinai | جنائي | Jinai | *Criminal* |
| ✓ Adhabu | تاديب | tadib | *Punishment* |
| ✓ Hoja | حجة | Hoja | *Argument* |
| ✓ Dalili | دليل | dalil | *Evidence* |
| ✓ Rushwa | رشوة | Rashwa | *Bribery* |
| ✓ Wakili | وكيل | wakil | *Advocate* |
| ✓ Ufilisi | افلاس | Iflas | *Bankraupcy* |
| ✓ Dhambi | دنب | danb | *Sin* |
| ✓ Uharibifu | مضرة | kharab | *Damage* |
| ✓ Taarifa | معرفة | taarifa | *Information* |

*Chanzo: Abdelaatif (2024)*

## 13. Hitimisho

Mwisho, tunaweza kusema kwamba vipengele vya kitamaduni katika methali zinazoakisi tamaduni zote mbili zinaonekana wazi katika nyanja zote zilizotajwa katika makala hii ambazo ni nyanja za familia na haki. Hii inaonyesha wazi uhusiano wa kihistoria kati ya tamaduni hizi mbili kwani kufanana kuonekana si tu katika maisha yao ya kila siku (familia) bali pia katika hisia na imani zao (haki). Uelewa huu wa kitamaduni na mwingiliano wa kijamii unaashiria hisia fulani ya ushirikiano kati ya Waarabu na Waswahili kwa ujumla, kuonyesha utambulisho wao wa kitamaduni na kijamii, kwa lengo la kujenga maendeleo ya pamoja ya kupitia historia yao ya pamoja ya kitamaduni.

## 14. Marejeleo


[1]. Agha, A. (2007). *Language and social relations.* Cambridge University Press.

[2]. Ake, C. (2017). Justice as equality. In *Justice*. Routledge (pp. 121- 141).

[3]. Black, M. (1973). Meaning and intention: An examination of Grice's views. *New Literary History*, *4*(2),257–279. https://doi.org/10.2307/468477

[4]. Bräger, I. (2020) About Grice's notion of sentence-meaning and how it contrasts with speaker-meaning. GRIN Verlag.

[5]. Campbell, S., Greenwood, M., Prior, S., Shearer, T., Walkem, K., Young, S., … Walker, K. (2020). Purposive sampling: complex or simple? Research case examples. *Journal of Research in Nursing,* 0 (0), 1-10.

[6]. Condon, E. C. (1973). *Introduction to Cross-Cultural Communication.* Rogers University Press.

[7]. Crystal, D. (1985). *Linguistics.* Penguin Books.

[8]. Crystal, D. (1987). *The Cambridge encyclopedia of language.* Cambridge University Press.

[9]. Crystal, D. (2008). *A dictionary of linguistics and phonetics (6th ed.).* Blackwell.

[10]. Grice, H. P. (1957). Meaning. *The Philosophical Review, 64,* 377- 88.

[11]. Grice, H. P. (1969). Utterer's meaning and intentions. *The Philosophical Review*.

[12]. Harries, L. (1964). "The Arabs and Swahili culture" Journal of the International African Institute, 34(3), 224-229.

[13]. Jiang, W. (2000). The relationship between culture and language. *ELT Journal*, *54*(4), 328-334.

[14]. Johnson, L., Radesky, J., & Zuckerman, B. (2013). Cross-cultural Parenting Reflections on Autonomy and Interdependence. *Paediatrics, 131 (4),* 631– 633.

[15]. Kelly S (2010) Qualitative interviewing techniques and styles. In: Bourgeault I, Dingwall R and de Vries R (eds) *The Sage Handbook of Qualitative Methods in Health Research*. Thousand Oaks: Sage Publications.

[16]. King'ei, K. G., & Ndalu, A. E. (1989). *Kamusi ya methali za Kiswahili*. East African Publishers.

[17]. Kingei, G. K. (1992). *Uhakiki wa nthimo (Methali) za kikamba:(kwa kufuatisha misingi ya Methali za Kiswahili)* [Unpublished doctoral dissertation] University of Nairobi.

[18]. Kuo, M. M., & Lai, C. C. (2006). Linguistics across cultures: The impact of culture on second language learning. *Online Submission*, *1*(1).

[19]. Lunde, P. & J. Wintle. (1984). *A Dictionary of Arabic and Islamic Proverbs.* Routledge.

[20]. Mtesigwa, G. K. (2013). *Kuchunguza matumizi ya methali katika jamii ya wanyiramba.* Chuo Kikuu Huria Tanzania. [Haijachapishwa]

[21]. Mwaliwa, H. C. (2018). “Modern Swahili: The integration of Arabic culture into Swahili literature” *Tydskrif Vir Letterkunde 55(2),* 120 - 133.

[22]. Mwashota, P. (2017). Dhima za mbinu linganishi katika kuhusisha lugha na lahaja. *Kioo cha Lugha, 15 (1),* 75–88.

[23]. Mwita, L. C. (2009). “The adaptation of Swahili loanwords from Arabic: A constraint-based analysis” *The Journal of Pan African Studies, 2(8),* 46 – 61.

[24]. Nam, C. B. (2004). The concept of the family: Demographic and genealogical perspectives. *Sociation Today*, *2*(2), 1-9.

[25]. Olaniran, B. A., & Roach, K. D. (1994). Communication Apprehension in Nigerian culture. *Communication Quarterly*, *42,* 379–389.

[26]. Palinkas LA, Horwitz SM, Green CA, et al. (2015) Purposeful sampling for qualitative data collection and analysis in mixed method implementation research. *Administration and Policy in Mental Health and Mental Health Services Research* 42(5): 533–544.

[27]. Sini, I. & M. Soulaiman. (2010). *Dictionary of Arabic Proverbs*. Noor Book.

[28]. Shembilu, M. M. S., (2015). Mapokezi ya kisemantiki ya nomino za mkopo katika Kiswahili: Mifano kutoka nomino zenye asili ya kiingereza na kiarabu. *Kioo Cha Lugha. 13(1),* 145 – 156.

[29]. Tannen, D. (2006). *Language and Culture*. Cambridge University Press.

[30]. Versteegh, K. (2001). Linguistic contact between Arabic and other languages. *Arabica, 48(4).* 470-508.